



TANESCO Makao Makuu, S.L.P. 453, Dodoma, Tanzania, Simu +255 026 2323456/7

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### TANESCO NA MASDAR ZA SAINI MAKUBALIANO YA KUENDELEZA MIRADI YA NISHATI JADIDIFU NCHINI

**AGOSTI 04, 2022.**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Masdar inayomilikiwa na Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu wamesaini makubaliano ya kuendeleza nishati ya jadidifu nchini (Joint Development Agreement).

Hafra hiyo imefanyika kando ya Kongamano la Kimaitaifa la Nishati linalofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku mbili na kushuhudiwa na Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba.

Makubaliano hayo yanalenga uendelezaji wa nishati jadidifu ambapo utekelezaji wa miradi hiyo utafanyika kwa awamu mbalimbali ikiwa na lengo la kufikia hadi Megawati 2000 za umeme nchini.

Akizungumza katika hafra hiyo Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba amesema kuwa tukio la utiaji saini makubaliano hayo ni matunda ya ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyofanya mapema mwaka huu katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E.).

Kwa upande, wake Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande amesema makubaliano haya kati ya TANESCO na kampuni ya Masdar yataleta mapinduzi makubwa katika uendelezaji wa nishati jadidifu nchini.

"Mkataba tunaosaini leo utahusisha uendelezaji wa nishati ya jadidifu hususan nishati ya jua, ambapo katika mradi wa awamu ya kwanza tunatarajia kuzalisha takribani Megawati 600 za umeme wa jua, na tutaendelea na miradi mingine hadi kufikia Megawati 2000," amesema Maharage.

Naye Mkuu wa Uendelezaji Biashara na Uwekezaji wa Masdar, Abdulla Zayed amesema kuwa miradi iliyopo kwenye makubaliano hayo uendelezaji wake unategemea kufikisha Megawati 5000 hadi kufika mwaka 2025.

Utekelezaji wa mkataba huu utasaidia kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo mseto nchini.

Imetolewa Na;  
OFISI YA UHUSIANO,  
TANESCO- MAKAO MAKUU.  
DODOMA